JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
Simu: 0734005777

# TANGAZO

## MABADILIKO YA TAREHE ZA MTIHANI WA USAJILI OKTOBA 2024

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu watahiniwa wote waliofanya maombi ya mtihani wa usajili kwa mwezi Oktoba 2024 kuwa kuna mabadiliko kidogo ya tarehe za mtihani wa usajili kama ifuatavyo:

| NGAZI YA ELIMU | TAREHE YA MTIHANI | |
|---|---|---|
| | NADHARIA (THEORY) | VITENDO (PRACTICAL) |
| ASTASHAHADA (CMLS) | 08.10.2024 | 09.10.2024 |
| STASHAHADA (DMLS) | 15.10.2024 | 16.10.2024 |
| SHAHADA (BMLS) | 22.10.2024 | 23.10.2024 |

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

1. Watahiniwa wote wanatakiwa kufika katika chumba cha mtihani siku ya kwanza ya mtihani kabla ya saa 2:00 asubuhi kwa ngazi zote katika tarehe husika ya mtihani na ngazi husika. Hata kama atafanya mtihani wa vitendo pekee anatakiwa awepo siku ya kwanza kwa ajili ya uhakiki.
2. Kila mtahiniwa atalazimika kufika na **NYARAKA HALISI** zifuatazo kwa siku zote za mitihani;
   - Cheti cha Usajili wa awali (Provisional Registration)
   - Kitambulisho cha Serikali (NIDA, Kitambulisho cha mpiga kura, leseni ya udereva au pasi ya kusafiria)
   - Ikiwa mtahiniwa hana kitambulisho tajwa hapo juu atatakiwa kuwa na barua kutoka serikali ya mtaa ya kumtambulisha ikiwa na picha iliyongwa muhuri
3. Mtahiniwa ambaye hatafika na nyaraka hizo **"HATARUHUSIWA KUFANYA MTIHANI"**. Nyaraka laini (Soft Copy) au za kudurufu hazitakubaliwa.
4. Vitu vingine vya kufika navyo kwenye chumba cha mtihani ni Koti jeupe la maabara, kalamu ya wino nyeusi au ya bluu.
5. Aidha, Watahiniwa wanakumbushwa kuwa namba za mitihani zinapatikana kwenye akaunti ya *hprs.moh.go.tz* ya kila mtahiniwa. Kama umefanya malipo hujapata namba ya mtihani tafadhali tuma ujumbe mfupi kwenye **0734005777** au Barua pepe mitihani.hlpc@afya.go.tz
6. Mtahiniwa ambaye aliomba *control number* na hajalipia, anasisitizwa hadi ifikapo 20.09.2024 awe amefanya malipo, baada ya hapo hataruhusiwa kufanya mtihani hadi kipindi kingine.

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara linaomba radhi na linawatakia Mtihani mwema.

Imetolewa na
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
19.09.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
19 SEP 2024
P.O.Box 743
DODOMA